**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU HALI YA UREJESHAJI WA TAMKO LA RASILIMALI NA MADENI NA MFUMO WA UJAZAJI FOMU ZA TAMKO KWA NJIA YA MTANDAO. TAREHE 21 DESEMBA, 2023.

*Imeandaliwa na:-*

*Ofisi ya Rais,*
*Sekretarieti ya Maadili ya*
*Viongozi wa Umma,*
*S. L. P 225,*
*DODOMA.*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU HALI YA UREJESHAJI WA TAMKO LA RASILIMALI NA MADENI NA MFUMO WA UJAZAJI FOMU ZA TAMKO KWA NJIA YA MTANDAO. TAREHE 21 DESEMBA, 2023.**

**Ndugu Wanahabari,**

Karibuni sana hapa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni Idara ya Serikali inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 132(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa ipasavyo na viongozi wote wa umma.

Kwa Mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995, Sekretarieti ya Maadili ina jukumu la kukuza na kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma nchini ili kuhakikisha kwamba Viongozi wa Umma wanakuwa na tabia na mwenendo wa kimaadili.

Aidha, kifungu cha 19 cha Sheria ya Maadili kinaipa Sekretarietii ya Maadili wajibu wa;

1. Kupokea taarifa na tuhuma za ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma;
2. Kuchunguza tuhuma za ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma;
3. Kupokea matamko ya rasilimali na madeni yanayotakiwa kutolewa na Viongozi wa Umma;
4. Kufanya uhakiki wa matamko yaliyotolewa kwa mujibu wa Sheria;
5. Kuanzisha na kufanya uchunguzi wowote wa tuhuma za ukiukwaji wa maadili yaliyobainishwa na Sheria;
6. Kutoa elimu ya maadili kwa Viongozi wa Umma;
7. Kufanya tafiti kuhusu hali ya maadili nchini;
8. Kutoa ushauri katika masuala yanayohusu maadili nchini; na
9. Kuweka mikakati ya kukuza maadili nchini.

**Ndugu Wanahabari,**

Hadi kufikia tarehe 20/12/2023, Jumla ya Viongozi wa Umma **2,475** kati ya **15,762** ndio waliowasilisha Tamko lao la Rasilimalii na Madeni kwa Kamishna wa Maadili. Idadi hii ni sawa na asilimia **16** ya viongozi wote wanaopaswa kuwasilisha Tamko la Rasilimali na Madeni kwa mujibu wa Sheria. Zimebaki siku 10 tu ifike tarehe ya mwisho kwa Viongozi wa Umma kuwasilisha Tamko lao la Mwaka.

Hivyo, napenda kuwakumbusha Viongozi wote wa Umma nchini kuzingatia matakwa ya Katiba na Sheria ya Maadili ikiwa ni pamoja na kuwasilisha Tamko la Rasilimali na Madeni la mwisho wa Mwaka ifikapo tarehe 31 Desemba.

**Ndugu Wanahabari**,

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Phillip Mpango, Makamu wa Rais, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Viongozi wengine wa Umma waliokwisha timiza takwa hili la kisheria kwa kuwasilisha Matamko yao ya Rasilimali na madeni kwa Kamishna wa Maadili.

Nawasihi Viongozi wengine wa Umma ambao bado hawajawasilisha Matamko yao wakiwemo waliotamkwa katika Tangazo la Serikali Na. 857 la tarehe 24.11.2023 kuwa tangu siku ya tangazo hilo, wanawajibika kutimiza masharti yote ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ikiwemo kuwasilisha Matamko yao kwa Kamishna wa Maadili.

**Ndugu Wanahabari**,

Viongozi wawasilishe nakala halisi (original copy) katika ofisi zetu za hapa Makao Makuu Jengo la PSSSF Kambarage, Barabara ya Jakaya Kikwete - Dodoma, Ofisi za Kanda ya Kati zilizoko Viwanja vya Nanenane – Dodoma, Ofisi za Kanda Maalum Dar Es Salaam zilizoko Barabara ya Ohio karibu na Benki ya CRDB Holland House, Dar Es Salaam, Ofisi za Kanda ya Kaskazini zilizoko katika Jengo la Hazina – Arusha, Ofisi za Kanda ya Ziwa zilizoko Jengo la NSSF, Mtaa wa Kenyatta - Mwanza, Ofisi za Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zilizoko Jengo la NHIF – Mbeya, Ofisi za Kanda ya Mashariki zilizoko Jengo la NSSF –

Morogoro, Ofisi za Kanda ya Magharibi zilizoko Mkabala na Hoteli ya Orion – Tabora na Ofisi za Kanda ya Kusini zilizoko Jengo la Maadili – Mtwara, Mtaa wa Chikongola Barabara ya TANU. Aidha, kiongozi anaweza pia kuwasilisha Tamko kwa njia ya posta kupitia "registered mail" ikiwemo "ems."

**Ndugu Wanahabari**,

Kutokana na Mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, tumeanza kupokea Matamko kwa njia ya mtandao yaani '*Online Declaration System'* - ODS. Kiongozi ambaye hata weza kufika kwenye ofisi zetu, anaweza kujaza kwa njia ya Mtandao.

Hivyo, Viongozi wa Umma wanaweza kuingia katika mfumo kwa anuani https://ods.maadili.go.tz au kupitia Tovuti ya www.maadili.go.tz na kubonyeza neno ODS. Hapo wataingia moja kwa moja kujaza na kutuma Tamko bila wasiwasi.

Mfumo huu wa ujazaji fomu kwa njia ya mtandao utawawezesha Viongozi kujaza matamko yao kwa urahisi na kwa usahihi zaidi popote pale watakapokuwa iwe ndani au nje ya nchi. Nasi tutayapata haraka.

Mfumo huu wa ODS unamsaidia Kiongozi kutosafiri mwendo mrefu na kumpunguzia gharama za kupakua fomu za tamko kuzijaza na kuzituma kwa njia ya posta ambapo hutumia fedha na muda mrefu kufika katika ofisi zetu.

**Ndugu Wanahabari**,

Ujazaji wa Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya Mtandao utaepusha upotevu wa fomu katika zoezi la urejeshaji unaotokana na usafirishaji kwa njia ya posta au katika vyombo vingine vya usafiri.

Mfumo huu pia utaondoa uwezekano wa kupokea Matamko kutoka kwa watumishi ambao sio Viongozi kwa Mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995. Kiongozi atakayejaza Tamko atakuwa ametengenezewa akaunti na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma hivyo matamko yatakayopokelewa yatakuwa ya Viongozi wanaowajibika na Sheria ya Maadili na si vinginevyo.

Hivyo basi, baada ya kuanzisha mfumo huu, Viongozi wote wanaoteuliwa/wanaopandishwa vyeo na kuwajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, na wanaokoma uongozi kwa sababu yoyote ile wanapaswa kutuma taarifa zao Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kupitia anuani ya barua pepe "helpdesk@maadili.go.tz" ili waweze kutengenezewa akaunti za kuingilia katika mfumo huo.

**Ndugu Wanahabari**,

Taarifa zinazotakiwa kutumwa na viongozi ni Majina Matatu ya Kiongozi (Kwa kuanzia na jina la Kwanza, Kati na Ukoo), Namba ya (za) **simu ya mkononi,** Barua pepe binafsi ya kiongozi, Taasisi anayofanyia kazi, Cheo/Wadhifa wa kiongozi na tarehe ya uteuzi/kuchaguliwa katika wadhifa/cheo husika.

Viongozi wapya watapaswa kuwasilisha taarifa zao ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kuteuliwa/kuchaguliwa au kupandishwa cheo. Viongozi watatumiwa taarifa za siri kwa njia ya ujumbe mfupi kupitia simu zao za mkononi na barua pepe zitakazomuwezesha kuingia katika mfumo wa ODS**.** Zoezi hili limekwisha anza, wapo viongozi ambayo tumekwisha watumia taarifa kupitia simu zao za Mkononi. Kwa ufafanuzi na mawasiliano zaidi, Kiongozi anaweza kupiga simu ya mezani namba **+**255 26 2160199 au simu ya mkononi namba 0734 101040.

**Ndugu wanahabari**,

Ikumbukwe kwamba kwa kuzingatia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kifungu cha 9(1)(b) kinamtaka Kiongozi wa Umma kila mwisho wa mwaka kabla ya tarehe 31 Desemba, kuwasilisha Tamko lake kwa Kamishna wa Maadili linaloonyesha Rasilimali zake, au mume au watoto wake wenye umri usiozidi miaka kumi na minane (18) ambao hawajaoa au kuolewa.

Kwa kuzingatia kifungu cha 9(1)(a) na (c) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kinawataka Viongozi wapya waliopewa wadhifa ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupewa wadhifa huo, kujaza fomu za tamko na kuziwasilisha kwa Kamishna wa Maadili. Aidha, mwisho wa kutumikia wadhifa wake Kiongozi anatakiwa pia kujaza fomu za tamko la rasilimali na madeni yake na kuzituma kwa Kamishna wa Maadili.

**Ndugu Wanahabari**,

Napenda kuchukua fursa hii tena kuwakumbusha Viongozi wote wa Umma kuwa ni kosa kwa Mujibu wa Kifungu cha 16 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Kiongozi kushindwa kutoa tamko lake la rasilimali na madeni bila sababu za Msingi au, kuchelewesha kuwasilisha Tamko la Rasilimali na Madeni bila kuwa na sababu ya msingi au kutoa Tamko chini ya fungu la 9 akijua ni la uongo au potofu katika kipengele chochote muhimu.

**Ndugu wanahabari,**

Mwisho, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inafarijika sana kwa ushirikiano mkubwa tunaoupata kutoka kwa vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini na tunaomba ushirikiano huu uendelee ili kuhakikisha Taifa linakuwa na Viongozi waadilifu.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**

Waziri Y. Kipacha

**KATIBU, UKUZAJI WA MAADILI**